

1013/1 KISWAHILI
KARATASI YA 1
SAA 2
KARATASI YA 1 MWONGOZO
MACHI 2019

1. INSHA

1. (a) Hii ni insha ya maelezo.

- Ateue kichwa mwafaka kinacholenga kile anachoeleza.
- Itangulizwe kimuhtasari kwa sentensi inayobainisha mahali/kitu/jambo au MTU anayekusudiwa katika maelezo.
- Maelezo yatolewe kwa mpangilio wenye mantiki.km huanzia mambo mepesi hadi magumu ya karibu hadi mbali n.k.
- Mwanafunzi afafanue zaidi maelezo katika utangulizi kwa kuzingatia mantiki
- Matumizi ya msamiati yaandamane na yale yanayoelezwa.
- Katika uhitimisho sentensi ioneshe kutimia kwa maelezo au kwa kurejelea sifa za kinachoelezwa.

- Hatua za kuimarisha ufasaha wa lugha ya Kiswahili ni kama zifuatazo:

- Kuunda kamati za kushughulikia lugha
- Kuunda sera ya lugha
- Kuimarisha ufundishaji wa Kiswahili
- Kuimarisha matumizi ya Kiswahili sanifu katika mawasiliano
- Kutoa tuzo kwa watumiaji wa lugha sanifu
- Kukuza istilahi na msamiati
- Kuunda warsha/semina za Kiswahili

(b) Insha hii ifuate mtindo wa kumbukumbu.

1. Kichwa kionyeshe wanaokutana, mahali pa mkutano, tarehe na saa ya kufanyika mkutano huo.
2. Orodha ya waliohudhuria
3. Orodha ya waliotuma tuima udhuru wa kutohudhuria
4. Orodha ya wasiohudhuria na hawakutuma udhuru(optional)
5. Orodha ya waalikwa, ikiwa wapo.
6. Ajenda ya mkutano:
 - a) Pawe na maelezo kuhusu ufunguzi wa mkutano ambao huweza kuwa maombi
 - b) Maelezo kutoka kwa mwenyekiti
Kusoma na kudhibitisha kumbukumbu za mkutano uliopita.
 - c) Masuala ibuka – hutokana na mkutano uliotangulia.
 - d) Rekodi ya mkutano wa sasa na maamuzi ya masuala makuu ya ajenda km;
 - Uanachama
 - Kuandaa makongamano
 - Kuwatuza wanafunzi bora
 - Miradi
 - Masuala mengineyo
 - Kufunga mkutano

Tanbihi: idadi ya maneno katika kumbukumbu huanza kuhesabiwa wakati unapoanza kufafanua ajenda za kumbukumbu.

- Mambo yaandikwayo yawe rasmi

- (c) - Hii ni insha ya methali
- kichwa cha insha huwa ni methali uliyopewa
 - kisa kinachotungwa sharti kiwe na maana ya ndani na ile ya nje.
 - Mwanafunzi atunge kisa ambacho kinaonesha mtu ambaye anakiri anapokosa.
- (d) _ Hii ni insha ya mdokezo wa awali
- Kisa kitakachoandikwa kianze na kuoana na kidokezo alichopewa.
 - Aonyeshe ni kipi kilichotokea hadi kufedheheka jinsi ya kutoisahau siku hiyo.
 - Kichwa kisawiri yale yaliyodokezwa.
 - Utangulizi: Uendelezwe ili kutoa taswira ya kile anachotazamia kukiwasilisha.
- _Mwili wa insha: Atoe kisa kinachooana na utangulizi.
- Katika hitimisho: Insha huhitimishwa kwa kauli ya masimulizi. Anaweza kutoa muhtasari wa kisa au funzo.

2. UFAHAMU

- a) - Chakula chenye lishe bora na faida tele kwa mwili
- Ushirikiano wa karibu na jamaa na majirani
 - Watu kuwajua na kuwatambua majirani
 - Watu kuwajua na kuwatambua jamaa na marafiki
 - Kutambua mizizi ya ukoo
 - Kuamkuana na kujuliana hali
 - Hakuna misongamano ya magari na kupoteza wakati (zozote 6. Alama 1 kila hoja $6 \times 1 = 6$)
- b) i) Mji una raha zake kama vile;
- maendeleo makubwa yanayoashiriwa na wingi wa magari
 - uwezo mkubwa wa kifedha
 - usafiri wa haraka. (zozote 3, alama 1 kila moja 3×1)
- ii) -Mjini jamaa hawajuani
- watu hawatangamani
 - watu hawashirikiani
 - watu hawasaidiani
 - watu hawajuliani hali. (zozote 3 alama 1 kila moja 3×1)
- c) i) Nguo zake zilikuwa kuukuu na zilizopoteza rangi na kuanza kuraruka.
- ii) Kuwatembelea wakwe na kuwakuta hawajajitayarisha kwa makaribisho yakufaayo hali inayowapa aibu.
- iii) Salimiana kwa kukumbatiana kwa mikono aghalabu vifua vikielekeana
- iv) Furaha yote iligeuka maudhi, huzuni na uchungu
- v) Chafukiwa na moyo nusra utapike, pata kizunguzungu. (alama 1 kila moja $5 \times 1 = 5$)
- d) Methali: -Kwenda kwa wakwe uwapate wanakwenda uchi.
- Msemo: -Ona kisunzi
- Tashbihi: -Mmekuwa mithili ya miti
- Msemo/useja: - alichukua bilahuri, akapiga tama, kisha akaendelea kunofua sima.
- Tashhisi – barabara hizi zimewameza. (zozote tatu, $3 \times 1 = 3$)

MATUMIZI YA LUGHA

3. a) i) Kipasuo au kizuiwa ni sauti ambayo inapotamkwa hewa huzuiliwa kabisa kisha ikaachiliwa kwa nguvu. (al.1)

ii) Kiyeyusho/nusu irabu ni sauti ambayo inapotamkwa hewa haizuiliwi kama ilivyo katika konsonanti zingine. Kutamka kwake kwa karibiana zaidi na kwa irabu. (al.1)

b) Halati wa akina Maria huishi na wajomba zetu. (al. 2)

c) Kikombe **kicho hicho** ndicho cha dhahabu. (al.2)

d) Kidani – nomino mahsusi/nomino ya pekee.

Mwanariadha – nomino ambata

Baraza la wazee – nomino ya jamii/nomino ya makundi. (3x1 alama 3)

e) Sentensi idokeze matumizi ya ‘ku’ yafuatayo:

-kuunda vitenzi jina/vitenzi nomino k.m. ku-cheza

- nafsi ya pili umoja/mtendewa k.m. **nakupenda**

- kuonyesha mahali – mahali **kunakofaa**

- kuonyesha wakati katika ukanusho wa wakati uliopita k.m. **sikufika**

- kuonyesha vitenzi vya silabi moja. **kula** (al. 2)

f) Shingo ya ng’ombe huyu ni ndefu mno. (al.2)

g) Atunge sentensi zenye viunganishi: wala, au, ama

K.m. Siji wala simwaliki

-Atakula wali au ugali

-Ama usome au uandike. (al. 2)

h) i) Maneno ya silabi za konsonati, konsonanti, irabu.

- Mfti - mu-fti

- Maktaba – ma-kta-ba

- Shukrani – shu-kra-ni. (1x1=al.1)

ii) Konsonanti, konsonanti, nusu irabu, irabu

- jangwa – ja-ngwa

- tengwa – te-ngwa

- chungwa – chu-ngwa. (1x1= al. 1)

i) –Sentensi yenye kitenzi, kirai husishi


–Amesimama kando ya barabara

- Alisafiri kwa ndege

- Alikeripiwa na mamake

- Paka yuko juu ya meza. (yeyote 1x2= alama 2)

j) Sisi tunasoma lakini wao wamelala kabisa.



k) Majukumu ya mofimu.

Wa – kiina/nafsi ya tatu let – mzizi/shina.

Li – wakati uliopita a - kiishio

Cho- kirejeshi

Ki – kiambishi ngeli/kiwakilishi nomino. (1/2 x 6=alama3)

l) “Nitasomea mtihani huu leo jioni”, Kirima alisema. (al. 2)

m) i) ‘Po’ ya wakati – Nitakusaidia utakaporudi.

ii) ‘Po’ ya mahali – Alipokwenda sipajui. (2x1= alama 2)

n) Sijaja kuomba msamaha. (1x1 = alama 1)

4. a) Sentensi idokeze maana zifuatazo za neno: sita.

- tarakimu/idadi ya hesabu

- acha kulifanya jambo baada ya kutia nia ya kulifanya au ya kulianza.

- sema kwa kukokoteza maneno

- ingiwa na shaka au wasiwasi, kosa kuwa na msimamo maalum, kutokuwa na hakika.

b) Mchana (al.1)

c) i) Roshani (al 1)

ii) Sia (al 1)

iii) Patasi/juba/chunusi au kekee (al.1)

iv) Wizara ya uchukuzi na miundo msingi. (al. 1)

v) Darubini. (al. 1)

d) saa tatu kasoro dakika tano alasiri. (al. 1)

o) e) Pweza (al.1)

p) Kifuku (al.1)

- q) Bikari (al.1)
- r) Utitiri (al.1)
- s) Zohali (al.1)
- t) Msaada wa mbali hauwezi kukuokoa au kuwa na manufaa. (al.2)
- u) Macho (al.1)
- v) Hudhurungi/kikahawia (al.1)
- w) Kifaduro (al.1)
- x) Masizi (al.1)

SEHEMU YA NNE: ISIMU JAMII (ALAMA 10)

5. a) Ni lugha ya wastani kutokana na lahaja mbalimbali za lugha. Ni lugha yenye msamiati unaoeleweka na wengi kimaana na kimatamshi kati ya watumizi wa lugha moja kuu. (alama 2)

b) -Mafunzo shuleni na katika taasisi ya kielimu.

- mitihani na utahini

- uchapishaji wa vitabu

- uandishi wa magazeti na majarida

- usawa wa matumizi kimaana na kimatamshi

- vyombo vinginevyo vya habari kama vile redio na runinga.

(zozote 4 alama 2 kila moja $4 \times 2 = 8$)